## MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI KILICHOKETI

## TAREHE 25.11.2021

# AGENDA

Agenda na 1: Kufungua Kikao

Agenda na 2: Kujadili taarifa kutoka kamati ya fedha uongozi na mipango juu ya fedha zilizopotelewa kutekeleza miradi ya maendeleo

Agenda na 3: Mengineyo

Agenda na 4: Kuahilisha Kikao

**AGENDA NA 1 KUFUNGUA KIKAO**

Mnamo saa nne kamili asubuhi Mwenyekiti alifungua kikao kwa kuwakaribisha wajumbe kushiriki kikao hiki cha bodi ya zabuni.

**AGENDA NA 2: KUJADILI TAARIFA KUTOKA KAMATI YA FEDHA UONGOZI NA MIPANGO JUU YA FEDHA ZILIZOPOTELEWA KUTEKELEZA MIRADI YA MAENDELEO (UVIKO)**

Katibu wa bodi alisoma taarifa kutoka FUM kuhusiana na upokeaji wa fedha ( UVIKO )kwa ajili ya kutekeleza miradi ya aendeleo katika Halmashauri yetu. Taarifa hiyo ilionyesha mapokezi ya fedha za kutekeleza miradi kama ifuatavyo.

| S/N | MAELEZO | IDADI | KIASI KILICHOPOKELEWA |
|---|---|---|---|
| 1. | Vyumba vya madarasa kwa shule za Sekondari | Vyumba 53 | 1,060,000,000/= |
| 2. | Miundombinu ya vyumba vya madarasa kwa kituo shikizi | Vyumba 2 | 40,000,000/= |
| 3. | Majengo ya huduma Dharura EMD | 1 | 300,000,000/= |
| 4. | Nyumba ya tumishi 3 kwa 1 | Nyumba 1 | 90,000,000/= |
| 5. | Ununuzi wa mashine za mionzi | 01 | 420,000,000/= |

Kikao hiki cha bodi kilijadili pia njia/mbinu itakayo weza kufanyika utekelezaji wa miradi hiyo.

Bodi ya zabuni baada ya majadiliano ilitoa kibali cha kutumia njia /approach ya Force Account kwa ujenzi wa vyumba vya madarasa 54 vya sekondari , miundo mbinu ya vyumba vya madarasa kwa kituo shikizi vyumba 2, Jengo la huduma ya dharura( EMD) na ujenzi wa vyumba vya watumishi 3 kwa 1

Pia kikao kiliamua Ununuzi wa mashine za mionzi zitumike kwa njia ya single source kwa kuwa wazabuni wanohusika na uuzaji wa mashine hizo ni wachache

**AGENDA NA 3:MENGINEO**

Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe kama walikuwa na mengineo ila hapakuwa na mengineo.

**AGENDA NA 4:KUHAIRISHA KIKAO**

Mwenyekiti alihairisha kikao mnamo saa tano kamili kwa kuwatakia utekelezaji mwema wa kazi zao na kuwaomba wajitume sana kutekeleza miradi hii kwa wakati.

Nice O. Msuya

**Kny:Katibu wa bodi**

Masau M. Koligo

**Mwenyekiti wa Bodi**

MAHUDHURIO BODI YA ZABUNI

| | JINA KAMILI | WADHIFA | SAINI |
|---|---|---|---|
| 1. | MASAU M KONGO M/KITI | [illegible] | |
| 2. | NICE OMARY MSUYA | Secretarity | |
| 3. | MARYCELINA, C. MBEHOMA | Mjumbe | |
| 4. | Angelo Kalolo | Mjumbe | |
| 5 | Mjairi B. Julius | Mjumbe | |